## Maswali

1. Baada ya miaka mbili Waisraeli walikuwa wamefika wapi?
2. Musa alituma wapelelezi wangapi?
3. Musa aliwambia wachunguze nini?
4. Wapelelezi walisafiri kwa muda gani?
5. Wapelelezi waliambia Waisraeli nini juu ya nchi?
6. Wapelelezi kumi walileta habari gani mbaya?
7. Nani aliambia Waisraeli waamini Mungu?
8. Waisraeli waliamua wafanye nini?
9. Mungu aliwaadhibu Waisraeli namna gani?
10. Watu wawili waliotoka Misri na kuenda kwa Nchi ya Ahadi ni nani?

## Majibu

1. Waisraeli walifika kwa mpaka wa Kanaani, Nchi ya Ahadi.
2. Musa alituma wapelelezi 12.
3. Kuchunguza nchi, mimea na watu.
4. Wapelelezi walisafiri nchini kwa siku arobaini.
5. Wapelelezi walisema nchi ilikuwa nzuri, mimea mizuri na matunda mingi.
6. Wapelelezi kumi walisema watu hao wana nguvu, kuna majitu na miji yao ni kubwa na kuta za nguvu.
7. Yoshua na Kalebu waliambia watu kuamini Mungu.
8. Waisraeli waliamua kuchagua kiongozi mwingine na warudi Misri.
9. Watasafiri jangwani kwa miaka 40. Hawataingia nchini.
10. Yoshua na Kalebu wataenda mpaka nchini kwa sababu waliamini Mungu.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2 Mwaka wa 1

# 23 Wapelelezi kumi na mbili

**Kwa Biblia** Hesabu mlango wa 13 na 14:1-39

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anauwezo wa kufanya kila kitu. Hakuna kisicho wezekana kwa Mungu. Tunapaswa kuamini Mungu, hata kama kuna shida kubwa atatusaidia.


## Somo

Waisraeli walisafiri jangwani kwa miaka mbili. Baadaye walifika kwa mpaka wa nchi ya Kanaani. Musa alisanya Waisraeli wote pamoja. Aliwambia kwamba wamefika nchi yenye Mungu aliwaahidi atawapa. Musa aliambia watu kwamba wamefika mwisho wa safari yao. Sasa wangeenda nchini na wajenge miji ya kuishi. Lakini kulikuwa na watu wanaoishi huko. Lazima wakae ngumu na ujasiri. Lazima waamini Mungu. Atawasaidia washinde na kupata nchi.

Musa alituma wapelelezi kumi na mbili mmoja kutoka kwa kila kabila ya Israeli. Musa aliwambia wapelelezi watembee nchi mzima wakipeleleza. Wachunguze nchi hiyo yote – Wapi penye miji zimejengwa. Ni watu gani waliishi huko? Nchi hiyo ina mali au la? Matunda gani inakua huko? Musa alituma wapelelezi kutazama nchi na wawe na ramani ya vilima, mito, misitu na milima. Wakirudi waambie watu kila kitu walichopata na kuona.

Wapelelezi walisafiri nchi nzima kwa siku arobaini. Walisafiri polepole kwa utaratibu. Hawakutaka wenyeji wawaone. Wapelelezi walisafiri juu ya vilima na ndani ya mabonde. Waliona miji na vijiji. Waliona mimea na matunda yanayokua kwa nchi. Walichunguza vile watu wanaishi. Walipomaliza kuchunguza, walirudi kambini na kuambia Waisraeli yote waliyoona.

Waisraeli walifurahi walipoona wapelelezi wamerudi. Musa alikusanya watu wote pamoja ili wasikie habari yenye wapelelezi walikuja nayo.



Wapelelezi walikuwa na mengi ya kusema. Walisema nchi ni nzuri sana – nchi inatiririka na maziwa na asali. Ilikuwa nchi ya mazao mengi. Ilikuwa na mimea na miti ya matunda mingi. Wapelelezi walileta mizabibu, komamanga na tini ya kuonyesha watu. Fungu moja ya zabibu ilikuwa kubwa na ingebebwa kwa vito na watu wawili. Waisraeli walifurahi kusikia habari njema juu ya nchi.

Lakini wapelelezi kumi hawakuamini Mungu. Walipea Waisraeli habari mbaya. Walisema, "Ni nchi nzuri lakini watu wanaoishi huko wana nguvu kuliko sisi. Wengine wao ni majitu. Watu wa nchi wanaishi kwa miji mikubwa iliyozungukwa na kuta za nguvu ya minara. Tunaogopa kwenda kuishi huko. Hatutaweza kupigana na hawa watu wa nguvu.

Waisraeli waliposikia haya, waliogopa. Hawakutaka kwenda kuishi kwa hiyo nchi. Wapelelezi wawili, Yoshua na Kalebu waliamini Mungu. Kalebu na Yoshua walipea watu moyo. Waliwambia, "Mungu ana nguvu kuliko majitu. Atatusaidia tushinde hiyo miji." Lakini Waisraeli hawakusikiliza. Walisahau miujiza yote yenye Mungu aliwafanyia. Hawakuamini Mungu. Walienda kwa mahema yao na kulia usiku kucha.

Ilipofika asubuhi Waisraeli walikuwa wamekasirika. Walitaka kupiga Musa na Haruni mawe. Waisraeli walikasirika kwa sababu walikuwa wamesafiri mwendo mrefu jangwani. Sasa wameogopa kwenda kwa nchi waliyoahidiwa na Mungu. Waisraeli waliamua kuchagua kiongozi mwingine awarudishe Misri.

Yoshua na Kalebu walijaribu kuwashawishi waamini Mungu. Mungu aliwaokoa kutoka Misri. Aliwasafirisha salama safarini. Aliwaahidi kuwapa nchi ya kuishi. Waisraeli wanatakiwa waamini Mungu. Lakini Waisraeli hawakusikiliza.

Papo hapo utukufu wa Mungu ulitokea maskani katikati ya kambi. Mungu alizungumza na Waisraeli kupitia kwa Musa. Mungu aliwambia kwamba kwa sababu wameogopa na hawakumwamini, hatawaruhusu kuenda kwa nchi ya ahadi. Wapelelezi walichukua siku arobaini kuchunguza nchi. Mungu aliwambia Waisraeli lazima warudi jangwani na wasafiri kule kwa miaka arobaini. Kwa kila siku yenye wapelelezi walichukua kuchunguza nchi, Waisraeli watachukua mwaka moja kukaa jangwani. Hiyo ilikuwa adhabu ya Mungu kwa sababu hawakumwamini.

Watu wenye hawakuamini Mungu watakufia jangwani. Hawataingia kwa nchi aliyowaahidi. Baada ya miaka arobaini, watoto wao na wajukuu wao pekee ndio watakuwa hai. Wataenda kwa nchi.

Waisraeli wote waliotoka Misri, ni Kalebu na Yoshua tu ndio wataenda kwa nchi. Kalebu na Yoshua waliamini Mungu. Mungu atawaweka hai kwa miaka yote arobaini. Wataenda kwa nchi kwa sababu waliamini na kutumaini Mungu.

Musa aliongoza Waisraeli kutoka kwa nchi ya ahadi. Walisafiri jangwani kwa miaka arobaini kabla ya kuenda na wafike nchini.